

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI
GREDI 4 - 2020
SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina

Jina la shule

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

Jumla ya alama = 50			
Viwango vya kutathmini			
Kuzidisha matarajio (50)	Kufikia matarajio (25 - 49)	Kukaribia matarajio (16 - 24)	Mbali na matarajio (0 - 15)

SEHEMU YA KWANZA

Kusikiliza na Kuzungumza.

(Alama 20)

i) **Soma maneno haya.**

Kizingiti	Tumbuu	Globu	Tendeguu	Kochi
Kinu	Mchi	Dari	Balbu	Sebuleni

ii) **Taja wanyama watano wanaofugwa nyumbani.**

<hr/> <hr/> <hr/>	<hr/> <hr/> <hr/>
-------------------	-------------------

iii) **Taja vifaa vitano vya nyumbani.**

<hr/> <hr/> <hr/>	<hr/> <hr/> <hr/>
-------------------	-------------------

SEHE MU YA PILI

KUSOMA

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata. (alama 10)

Shangazi yangu anaitwa Chaurembo. Zamani alifanya kazi katika hospitali. Aliacha kazi hiyo na kuanza biashara ya kuuza bidhaa sokoni. Biashara hiyo inamletea faida. Wanunuzi wanampenda sana. Anawauzia bidhaa kwa bei nafuu. Anawauzia pia bidhaa nzuri na halali.

Kibanda chake ni safi. Shangazi Chaurembo ni mwaminifu. Anatumia ratili kupima bidhaa zake. Anarudishia mnunuzi baki sahihi. Chaurembo ni muuzaji kwa mzuri wanunuzi wa bidhaa zake. Ni mfanyibiashara maarufu.

1. Shangazi yangu anaitwa nani? _____
2. Hapo zamani alifanya kazi wapi? _____
3. Chaurembo anatumia nini kupima bidhaa zake? _____
4. Taja sifa mbili za bidhaa ambazo shangazi Chaurembo anawauzia wanunuzi.
a) _____ b) _____
5. Sema ndio ama la.
 - a) Shangazi yangu anaitwa Chausiku. _____
 - b) Shangazi hakuacha kazi hospitalini. _____
 - c) Chaurembo huuza bidhaa sokoni. _____
 - d) Shangazi yangu ni mwaminifu. _____
 - e) Kibanda cha shangazi yangu si safi. _____

SARUFI

Kanusha maneno haya.

6. Anaimba - _____
7. Anakula - _____
8. Tulienda - _____
9. Watacheza - _____
10. Mlituburudisha - _____

Tumia viwakilishi 'mimi', 'sisi', 'wewe', au 'wao' kujaza pengo.

11. _____ unapenda somo lipi?
12. _____ ninasoma hadithi fupi.
13. _____ utaniletea maziwa kesho?
14. _____ tunakariri mashairi darasani.
15. _____ walikula chakula kitamu jana.

Andika wingi wa sentensi hizi.

16. Kitabu changu kimeraruka. _____
17. Mpira unachezwa. _____
18. Mtoto analia. _____
19. Ukuta umebomoka. _____
20. Kalamu imevunjika. _____

Andika kwa nambari.

21. Themanini na saba. - _____
22. Mia nne hamsini na sita. - _____
23. Mia saba na tisa. - _____
24. Tisini na nne. - _____
25. Elfu moja. - _____